# SISALANA TANZANIA COMPANY LIMITED

P. O . Box 342, TANGA, TANZANIA – Tel No. +255 272642130, +255 272642132, Email: info@sisalana.co.tz , Website: www.sisalana.co.tz

**STCL/TSB/47** **8 Februari 2023**

Mkurugenzi Mkuu,

Bodi ya Mkonge Tanzania,

S.L.P 270,

**TANGA**

**YAH: UWASILISHAJI WA TAARIFA YA UZALISHAJI KATIKA VIWANDA SABA VYA USINDIKAJI MKONGE VINAVYOMILIKIWA NA KAMPUNI YA SISALANA KWA KIPINDI CHA MWAKA 2022**

Tafadhali husika na somo tajwa hapo juu na barua yetu yenye Kumb Na STCL/TSB/27 ya tarehe 8 Machi 2022.

Katika utaratibu wake wa kufanya kazi kwa uwazi, Kampuni inapenda kuchukua fursa hii kuwasilisha taarifa ya utendaji wake katika viwanda vyake saba (Magoma Kulasi, Magoma Songea, Mwelya, Hale, Usambara, Magunga na Ngombezi) vinavyohusika na usindikaji wa majani ya Mkonge. Taarifa inaonyesha utendaji kuanzia Januari 2022 hadi Disemba 2022 kwa kulinganisha na utendaji wa mwaka 2021.

Wako katika maendeleo ya Mkonge.

**SISALANA (T) Co Ltd**

**Elizabeth J. Kalambo**

**Afisa Mtendaji Mkuu**

Nakala:

Mheshimiwa, Katibu Mkuu,

Wizara ya Kilimo,

P.O.Box 2182,

**40487 DODOMA**

Mheshimiwa, Mkuu wa Mkoa wa Tanga,

S.L.P 5095,

**TANGA**

Mheshimwa, Mkuu wa Wilaya,

Wilaya ya Korogwe,

**KOROGWE**

Mkurugenzi Mkuu,

Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii,

S. L. P 1322,

**DAR ES SALAAM**

**Mwenyekiti AMCOS (Mwelya, Ngombezi, Magunga, Hale na Magoma)**

Katibu,

Sisal Association of Tanzania (SAT),

**TANGA**

**TAARIFA YA UTENDAJI WA VIWANDA VYA KUSINDIKA MKONGE KWA KIPINDI CHA MWEZI JANUARI 2022 HADI DISEMBA 2022**

## 1.0 UTANGULIZI

Kampuni ya Sisalana ni moja ya kampuni za kitanzania ambayo inamilikiwa na mfuko wa hifadhi ya jamii (yaani NSSF) kwa asilimia 100%. Kampuni ya Sisalana ilianza shughuli zake ya utendaji tarehe 12. 03. 2021, Kampuni ya Sisalana inamiliki viwanda saba vya kuchakata Majani ya Mkonge (yaani kiwanda cha Magunga, Mwelya, Usambara, Hale, Ngombezi, Magoma Songea na Magoma Kulasi) ambapo majani hayo hutoka kwa wakulima kupitia usimamizi wa AMCOS tano (Magoma AMCOS, Magunga AMCOS, Hale AMCOS, Mwelya AMCOS, na Ngombezi AMCOS).

Ikumbukwe kwamba, Kampuni ya Sisalana ilianzishwa kwa lengo la kusimamia mali zote zilizochukuliwa na NSSF kutoka kwa Kampuni ya Katani baada ya kampuni tajwa kushindwa kulipa madeni yake kwa NSSF. Hivyo mali zote zilizokuwa dhamana ya mikopo iliyotolewa na NSSF kwa Kampuni ya Katani ikihusisha viwanda hivyo saba vya usindikaji vilichukuliwa na sasa vinasimamiwa na NSSF kupitia kampuni yake ya Sisalana.

Mara baada ya kuchukua mali hizo, kwa maelekezo ya Serikali NSSF haikupaswa kusimamisha shughuli za uzalishaji hivyo hatua za haraka zilichukuliwa ikiwemo kutengeneza mpango kazi wa muda mfupi kuendeleza uzalishaji katika kipindi cha mpito. NSSF ililazimika kuchukua hatua hii kwa sababu yenyewe katika uwekezaji hua kuna miongozo ya kuifuata inayotolewa na benki Kuu ya Tanzania na moja wapo ni kwamba lazima upembuzi yakinifu ufanyike kuangalia tija ya uwekezaji kabla ya kuweka. Hivyo mchakato wa kuanza kwa upembuzi yakinifu ulishafanyika na sasa upembuzi yakinifu ulifanyika na upo katika hatua za mwishoni.

Aidha, NSSF ilichukua hatua za haraka za kunusuru kazi ziendelee kwa kipindi cha mpito cha kusubiria upembuzi yakinifu ukamilike, hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kutoa mtaji kwaajili ya uboreshaji wa miundombinu ya uzalishaji ikiwemo ukarabati mkubwa wa Makorona ambao ulikua haujafanyika kwa zaidi ya miaka saba iliyopita; ujenzi wa vichanja vipya vya chuma ili kukidhi mahitaji halisi ya kila kiwanda na ukarabati wa vichanja vilivyokuwa vimeharibika; na kuboresha hali ya maslahi ya wafanyakazi ili kuwapa ari ya kufanya kazi kwa ufanisi ikiwemo kulipa stahiki zao kwa wakati, kulipa michango yao ya NSSF, kupata bima ya matibabu, kulipia kodi ya mapato, kuchangia Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF), kwa Chama cha Wafanyakazi (TPAWU) na kuwapatia vifaa vya kazi. Hadi taarifa hii inaandikwa ukarabati mkubwa wa makorona ulishafanyika kwa viwanda vyote isipokuwa Hale ambao AMCOS yao ilishauri tusubiri kidogo wafidie uzalishaji uliokuwa umepotea walipokuwa wamepata changamoto ya Korona kwa vipindi viwili tofauti. Taarifa kamili ya ukarabati wa Makorona nayo imeambatishwa kwaajili ya urahisi wa kurejea.

Taarifa hii imebeba utendaji wa viwanda saba vya kusindika mkonge vinavyomilikiwa na kampuni ya Sisalana katika kipindi cha mwezi Januari hadi mwezi Disemba 2022. Aidha taarifa hii itaonyesha pia ulinganisho wa uzalishaji ulio fanyika katika kipindi cha kipindi kama hicho kwa mwaka 2021 kabla ya kuanzishwa kwa Sisalana kwaajili ya kupima maendeleo ya usindikaji mkonge katika viwanda hivyo.

## 2.0 USINDIKAJI WA MAJANI YA MKONGE

### 2.1 LENGO LA USINDIKAJI NA MAFANIKIO

Kampuni inafanya kazi ya kusindika majani ya mkonge ambayo yanaletwa na wakulima kupitia AMCOS, hivyo utendaji wa usindikaji unategemea ushirikiano kati ya Kiwanda na AMCOS ambao wanaleta majani na Kiwanda kuhakikisha mitambo ipo sawa kusindika majani hayo. Hivyo taarifa ya utendaji katika eneo la usindikaji inaonyeshwa kwa kuangalia malengo ya Kampuni na hali halisi iliyojitokeza.

Katika kipindi cha mwezi Januari hadi mwezi Disemba 2022 kampuni ilikuwa na lengo la kusindika jumla **meta 232,623.20** kulainisha na kufunga **tani 6,646.38**. Uhalisia wa uzalishaji ni **meta 173,785.97** kati ya meta 174,229.04 zilizoletwa viwandani ambapo ni sawa na **asilimia 75** ya lengo na ni sawa na **asilimia 99.8** ya uhalisia. Kwa upande wa ulainishaji na ufungaji uhalisia ni **tani 5,747.39** sawa na **asilimia 86** ya lengo kwa kipindi cha mwezi Januari hadi Disemba 2022.

Taarifa imeambatanishwa kama ifuatavyo: -


(a) **Uzalishaji** -katika kipindi cha mwezi Januari hadi Disemba 2022 kiwanda cha Hale kimeongoza katika uzalishaji kwa kuvuka lengo lilokuwa limepangwa na Kampuni kwa kufikia 101.5% ya usindijaji. Aidha, Kwa kuzingatia hali halisi ya majani yaliyoletwa kiwandani na kusindikwa viwanda vilifanikiwa kusindika majani hayo kwa 99.8% ila kwa kuzingatia malengo viwanda vyote vimefikia lengo kwa wastani wa 78%. Kwaupande wa uzalishaji wa tani viwanda viliweza kufikia 86.47% ya lengo lililokuwa limepangwa na Kampuni. Takwimu za uzalishaji kwa viwanda vyote zimeonyeshwa hapo chini katika jedwali namba 1.


**Jedwali namba 1: Takwimu za Usindikaji, Ulainishaji na Ufungaji**

| PRODUCTION ARCHIEVMENT ANALYSIS | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2021 | | | | | 2022 | | | | |
| | TARGET | ACTUAL | | PERCENTAGE (%) OF | | TARGET | ACTUAL | | PERCENTAGE (%) OF | |
| FACTORY | | MTS REC | MTS DEC | MTS DEC V/S TARGET | MTS DEC V/S MTS REC | | MTS REC | MTS DEC | MTS DEC V/S TARGET | MTS DEC V/S MTS REC |
| HALE | 34,954.00 | 31,963.50 | 31,884.00 | 91.22% | 99.75% | 34,468.60 | 35,117.00 | 34,989.50 | 101.51% | 99.64% |
| NGOMBEZI | 31,874.00 | 25,198.00 | 25,155.50 | 78.92% | 99.83% | 33,055.40 | 25,664.50 | 25,690.50 | 77.72% | 100.10% |
| MAGUNGA | 32,244.00 | 25,891.50 | 25,780.50 | 79.95% | 99.57% | 31,220.40 | 23,729.50 | 23,809.00 | 76.26% | 100.34% |
| MAGOMA (KULASI & SONGEA) | 59,280.00 | 49,422.00 | 49,440.00 | 83.40% | 100.04% | 68,272.60 | 49,925.00 | 49,846.00 | 73.01% | 99.84% |
| MWELYA & USAMBARA | 57,750.00 | 35,460.41 | 35,450.66 | 61.39% | 99.97% | 65,606.20 | 39,793.04 | 39,450.97 | 60.13% | 99.14% |
| **TOTAL** | **216,102.00** | **167,935.41** | **167,710.66** | **77.61%** | **99.87%** | **232,623.20** | **174,229.04** | **173,785.97** | **74.71%** | **99.75%** |

| PRODUCTION ARCHIEVMENT ANALYSIS | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2021 | | | | 2022 | | | |
| FACTORY | TARGET | ACTUAL | | PERCENTAGE (%) | TARGET | ACTUAL | | PERCENTAGE (%) |
| | | BRUSHING | BALING | | | BRUSHING | BALING | |
| HALE | 1,001.75 | 1,023.30 | 1,008.55 | 100.68% | 980.38 | 1,124.80 | 1,114.75 | 113.71% |
| NGOMBEZI | 874.09 | 605.47 | 609.17 | 69.69% | 939.57 | 659.45 | 658.15 | 70.05% |
| MAGUNGA | 932.08 | 792.45 | 788.60 | 84.61% | 868.16 | 746.40 | 747.00 | 86.04% |
| MAGOMA (KULASI & SONGEA) | 1,724.45 | 1,945.50 | 1,945.50 | 112.82% | 1,993.41 | 1,962.90 | 1,962.90 | 98.47% |
| MWELYA & USAMBARA | 1,641.97 | 1,166.64 | 1,126.00 | 68.58% | 1,864.85 | 1,233.36 | 1,264.59 | 67.81% |
| **TOTAL** | **6,174.34** | **5,533.35** | **5,477.82** | **88.72%** | **6,646.38** | **5,726.91** | **5,747.39** | **86.47%** |

**Ufunguo:** MTS REC= Meta za majani ya Mkonge zilizofikishwa kiwandani; MTS DEC= Meta za majani ya Mkonge zilizosindikwa; Kipimo cha Ulainishaji na Ufungaji ni tani.


UZALISHAJI HALISI
MTS ZILIZOSINDIKWA
60,000.00
50,000.00
40,000.00
30,000.00
20,000.00
10,000.00
-
HALE
NGOMBEZI
MAGUNGA
MAGOMA (KULASI & SONGEA)
MWELYA & USAMBARA
2,021.00 31,884.00 25,155.50 25,780.50 49,440.00 35,450.66
2,022.00 34,989.50 25,690.50 23,809.00 49,846.00 39,450.97
Axis Title
2,021.00
2,022.00


UZALISHAJI (TANI)
TANI
2500
2000
1500
1000
500
0
HALE
NGOMBEZI
MAGUNGA
MAGOMA (KULASI & SONGEA)
MWELYA & USAMBARA
VIWANDA
ULAINISHAJI 2021
ULAINISHAJI 2022
UFUNGAJI 2021
UFUNGAJI 2022

### (b). Uzalishaji wa madaraja ya singa

Uzalishaji pia umezingatia madaraja ya singa yanayotokana na ubora wa majani yaliyosindikwa na umakini wa usimamizi wa wataalamu wa viwandani humo.

Ufanisi katika kuzalisha madaraja ya juu umeongezeka kwa kiasi kikubwa kwa mwaka 2022 ukilinganisha na madaraja ya Mkonge yaliyozalishwa mwaka 2021. Madaraja ya 3L, 3S haya yalizalishwa kwa uchache kabisa kwa mwaka 2021 kwa viwanda vyote ila kwa mwaka 2022 yamezalishwa kwa viwanda vyote kwa. Aidha uzalishaji wa madaraja ya mkonge ya chini ulipungua kwa kiasi kikubwa kwa kipindi cha mwaka 2022. Kwa ujumla kwa mwaka 2022 madaraja ya juu yapo kwa 85% ya uzalishaji wote ukilinganisha na 78% ya uzalishaji wa madaraja ya juu kwa mwaka 2021. Hii yote ni manufaa kwa mkulima kwani madaraja ya juu yanauzwa kwa bei ya juu ukilinganisha na madaraja ya mkonge ya chini.

Takwimu kamili za uzalishaji wa madaraja mbali mbali ya Mkonge inaonekana katika majedwali na 2 na 3 yanayofuta hapo chini.

**Jedwali namba 2: Uzalishaji wa madaraja ya Mkonge; Brushing- Ulainishaji, Baling-Ufungaji**

| | BRUSNHING BY GRADES | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| BRUSHING 2021 | FACTORY | 3L | 3S | UG | SS UG | TOW I | TOWII | UF | TOTAL |
| | HALE | 26.95 | 10.30 | 665.10 | 270.85 | 30.80 | - | 19.30 | 1,023.30 |
| | NGOMBEZI | 4.25 | 5.75 | 533.00 | 47.75 | 23.00 | 3.20 | 3.75 | 620.70 |
| | MAGUNGA | 156.85 | 24.55 | 503.15 | 70.05 | 34.55 | 0.90 | 2.40 | 792.45 |
| | MAGOMA | 2.25 | 0.50 | 1,528.25 | 341.00 | 36.00 | 1.00 | 36.50 | 1,945.50 |
| | MWELYA & USAMBARA | 37.70 | 20.50 | 774.65 | 289.09 | 39.40 | 1.22 | 4.08 | 1,166.64 |
| | **TOTAL** | **228.00** | **61.60** | **4,004.15** | **1,018.73** | **163.76** | **6.32** | **66.03** | **5,548.58** |
| | | | | | | | | | |
| BRUSHING 2022 | FACTORY | 3L | 3S | UG | SS UG | TOW I | TOWII | UF | TOTAL |
| | HALE | 40.55 | 17.15 | 893.25 | 126.35 | 29.85 | - | 17.65 | 1,124.80 |
| | NGOMBEZI | 2.75 | 18.00 | 514.50 | 83.80 | 34.00 | 3.40 | 3.00 | 659.45 |
| | MAGUNGA | 122.45 | 39.15 | 501.35 | 54.15 | 27.45 | 0.50 | 1.35 | 746.40 |
| | MAGOMA | 75.50 | 1.75 | 1,593.75 | 233.50 | 36.80 | 0.60 | 21.00 | 1,962.90 |
| | MWELYA & USAMBARA | 160.10 | 139.15 | 773.52 | 123.70 | 33.58 | 2.31 | 1.00 | 1,233.36 |
| | **TOTAL** | **401.35** | **215.20** | **4,276.37** | **621.50** | **161.68** | **6.81** | **44.00** | **5,726.91** |
| | | | | | | | | | |
| BALING BY GRADES | | | | | | | | | |
| BALING 2021 | FACTORY | 3L | 3S | UG | SS UG | TOW I | TOWII | UF | TOTAL |
| | HALE | 25.75 | 10.00 | 666.00 | 257.00 | 30.80 | - | 19.00 | 1,008.55 |
| | NGOMBEZI | 4.25 | 5.25 | 519.35 | 45.85 | 31.60 | 3.90 | 3.00 | 613.20 |
| | MAGUNGA | 160.00 | 24.00 | 501.25 | 67.35 | 32.60 | 0.90 | 2.50 | 788.60 |
| | MAGOMA | 2.25 | 0.50 | 1,528.25 | 341.00 | 36.00 | 1.00 | 36.50 | 1,945.50 |
| | MWELYA & USAMBARA | 33.50 | 15.25 | 808.55 | 217.90 | 35.00 | 12.40 | 3.40 | 1,126.00 |
| | **TOTAL** | **225.75** | **55.00** | **4,023.40** | **929.10** | **166.00** | **18.20** | **64.40** | **5,481.85** |
| | | | | | | | | | |
| BALING 2022 | FACTORY | 3L | 3S | UG | SS UG | TOW I | TOWII | UF | TOTAL |
| | HALE | 42.00 | 17.00 | 887.75 | 121.25 | 26.35 | 2.80 | 17.60 | 1,114.75 |
| | NGOMBEZI | 4.50 | 18.50 | 507.00 | 84.40 | 36.60 | 3.40 | 3.75 | 658.15 |
| | MAGUNGA | 122.75 | 39.25 | 501.50 | 54.25 | 27.50 | 0.50 | 1.25 | 747.00 |
| | MAGOMA | 75.50 | 1.75 | 1,593.75 | 233.50 | 36.80 | 0.60 | 21.00 | 1,962.90 |
| | MWELYA & USAMBARA | 154.75 | 135.45 | 781.90 | 127.95 | 57.09 | 7.20 | 0.25 | 1,264.59 |
| | **TOTAL** | **399.50** | **211.95** | **4,271.90** | **621.35** | **184.34** | **14.50** | **43.85** | **5,747.39** |

**Jedwali namba 3: Ufupisho wa Madaraja ya mkonge yaliyozalishwa katika Ulainishaji na Ufungaji**

| UZALISHAJI KWA MADARAJA YA SINGA | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| GRADES | 2021 (JANUARI-DESEMBA) | 2022 (JANUARI-DESEMBA) | ASILIMIA YA ONGEZEKO/PUNGUZO 2021 V/S 2022 | ASILIMIA YA MADARAJA YA SINGA KUTOKA KATIKA JUMLA YA UZALISHAJI | |
| | | | | 2021 | 2022 |
| 3L | 226.1 | 399.5 | 76.69% | 4.13% | 6.95% |
| 3S | 62.2 | 211.95 | 240.76% | 1.14% | 3.69% |
| **UG** | 3986.3 | 4271.9 | 7.16% | 72.77% | 74.33% |
| SS UG | 953.95 | 621.35 | -34.87% | 17.41% | 10.81% |
| TOW I | 167.486 | 184.34 | 10.06% | 3.06% | 3.21% |
| TOW II | 17.2 | 14.5 | -15.70% | 0.31% | 0.25% |
| UF | 64.58 | 43.85 | -32.10% | 1.18% | 0.76% |
| **TOTAL** | **5477.816** | **5747.39** | **4.92%** | **100.00%** | **100.00%** |

## 3.0. MAFANIKIO YA UZALISHAJI

Pamoja na kuwepo na changamoto za uzalishaji, Kampuni imefanikiwa katika maeneo yafuatayo:

a. Upande wa wadau wetu (AMCOS, wakulima na Serikali)
b. Upande wa kampuni

A. **Upande wa wadau wetu (yaani Mkulima na AMCOS)-**Pamoja na kusimamisha mitambo ya usindikaji kwa vipindi mbali mbali kupisha kipindi cha ukarabati mkubwa kampuni imeweza kugusa uchumi wa mkulima na vyama vyao vya Ushirika unaenda juu kutokana uzalishaji uliofanywa katika kipindi cha Sisalana kama ifuatavyo: -

- Kuongeza uzalishaji wa singa za majani ya mkonge (kwa kiasi na ubora)- kiasi cha tani 5,747.39 kimezalishwa kutoka jumla ya meta za majani ya mkonge 173,785.97 kwa mwaka 2022 ikiwa ni ongezeko la **tani 269.59** kipindi cha mwaka 2021.

- Ongezeko hilo pia limeenda sambamba na ongezeko la madaraja ya juu na kupungua kwa madaraja ya chini mfano katika kipindi cha 2021 uzalishaji wa 3L, 3S, UG ilikuwa ni asilimia 78.03% (3L=4.13%, 3S=1.14% na UG=72.77%) kutoka uzalishaji wa tani 5,477.80 ukifananisha na mwaka 2022 ambapo uzalishaji wa 3L,3S na UG ni jumla ya asilimia 84.97% (3L=6.95%,3S=3.69% na UG=74.33%) kutoka uzalishaji wa tani 5,747.39

- Kuongeza mapato ya mkulima na Vyama vya ushirika -kupitia usindikaji wa meta zaidi na madaraja ya 3L, 3S na UG kwa kiasi kikubwa ukilinganisha na uzalishaji wa mwaka 2022. Hali hii imepelekea pato ghafi la mkulima kuongezeka kwa **TZS 1.6 billion** ukilinganisha na kipindi cha mwaka 2021.

- Kuongeza mapato ghafi kwa AMCOS kwa **TZS 30.7 million** ukilinganisha na mapato yam waka 2021. AMCOS anakusanya mapato kwa kila meta inayopita kiwandani kwake kutoka kwa mkulima kwa TZS 5,000.00 kwa meta.

  Takwimu za mapato ghafi kwa vyama vya ushirika na Wakulima limeambatanishwa katika jedwali namba 4 na 5 hapo chini.

**Jedwali namba 4: Mapato ghafi ya AMCOS (Ongezeko la Sh 30,376,550)**

| MAPATO YA VYAMA VYA USHIRIKA VYA MKONGE (AMCOS) | | | | |
|---|---|---|---|---|
| AMCOS | 2021<br>5,000.00 | 2022<br>5,000.00 | TOFAUTI | ASILIMIA YA ONGEZEKO/PUNGUZO 2021 V/S 2022 |
| HALE | 159,420,000.00 | 174,947,500.00 | 15,527,500.00 | 9.74% |
| NGOMBEZI | 125,777,500.00 | 128,452,500.00 | 2,675,000.00 | 2.13% |
| MAGUNGA | 128,902,500.00 | 119,045,000.00 | (9,857,500.00) | -7.65% |
| MAGOMA | 247,200,000.00 | 249,230,000.00 | 2,030,000.00 | 0.82% |
| MWELYA & USAMBARA | 177,253,300.00 | 197,254,850.00 | 20,001,550.00 | 11.28% |
| **TOTAL** | **838,553,300.00** | **868,929,850.00** | **30,376,550.00** | **3.62%** |

**Jedwali namba 5: Mapato ya Wakulima (Ongezeko la Sh. 1,607,487,080.00)**

| GROSS REVENUES | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | GRADES | 3L | 3S | UG | SS UG | TOW I | TOW II | UF | TOTAL |
| 2021 | HALE | 104,697,500 | 38,500,000 | 2,435,550,000 | 798,091,250 | 61,135,000 | - | 29,325,000 | 3,467,298,750 |
| | NGOMBEZI | 17,425,000 | 20,212,500 | 1,894,485,000 | 142,727,600 | 62,684,000 | 5,950,000 | 4,500,000 | 2,147,984,100 |
| | MAGUNGA | 637,621,250 | 87,587,500 | 1,824,275,000 | 208,810,550 | 64,675,000 | 1,385,000 | 3,800,000 | 2,828,154,300 |
| | MAGOMA | 9,078,750 | 1,925,000 | 5,575,025,000 | 1,054,570,000 | 71,445,000 | 1,525,000 | 56,400,000 | 6,769,968,750 |
| | MWELYA & USAMBARA | 134,035,000 | 7,700,000 | 2,947,280,000 | 675,268,900 | 69,458,120 | 18,720,000 | 5,200,000 | 3,857,662,020 |
| | **TOTAL GROSS REVENUES** | 902,857,500 | 155,925,000 | 14,676,615,000 | 2,879,468,300 | 329,397,120 | 27,580,000 | 99,225,000 | 19,071,067,920.00 |
| | | | | | | | | | |
| | GRADES | 3L | 3S | UG | SS UG | TOW I | TOW II | UF | TOTAL |
| 2022 | HALE | 172,200,000 | 65,450,000 | 3,284,675,000 | 381,937,500 | 52,700,000 | 4,340,000 | 28,160,000 | 3,989,462,500 |
| | NGOMBEZI | 18,450,000 | 71,225,000 | 1,875,900,000 | 265,860,000 | 73,200,000 | 5,270,000 | 6,000,000 | 2,315,905,000 |
| | MAGUNGA | 503,275,000 | 151,112,500 | 1,855,550,000 | 170,887,500 | 55,000,000 | 775,000 | 2,000,000 | 2,738,600,000 |
| | MAGOMA | 309,550,000 | 6,737,500 | 5,896,875,000 | 735,525,000 | 73,600,000 | 930,000 | 33,600,000 | 7,056,817,500 |
| | MWELYA & USAMBARA | 634,475,000 | 521,482,500 | 2,893,030,000 | 403,042,500 | 114,180,000 | 11,160,000 | 400,000 | 4,577,770,000 |
| | **TOTAL GROSS REVENUES** | 1,637,950,000 | 816,007,500 | 15,806,030,000 | 1,957,252,500 | 368,680,000 | 22,475,000 | 70,160,000 | 20,678,555,000.00 |

- **Kwa upande wa Serikali;** Katika kipindi cha Januari 2022 hadi Disemba 2022, Kampuni imeweza kuchangia mapato kwa kulipa kodi (SDL, PAYE, Withholding na VAT) kiasi cha **TZS 1.04 billioni**. Aidha, kwa upande wa ajira Kampuni imeweza kuajiri wafanyakazi wa moja kwa moja wapatao **1,035** ikihusisha wa kudumu na wa muda mfupi. Hivyo Kampuni imechangia kuchochea uchumi wa Tanga kupitia uchangiaji wa mapato na kupunguza changamoto ya ukosefu wa ajira.

**B. Upande wa Kampuni**

- Kufanikiwa kuhakikisha huduma ya uzalishaji inaendelea kuwa ya uhakika na yenye ubora katika kipindi chote, hii imejidhihirisha kwenye ongezeko la uzalishaji kwa kiasi na ubora wa madaraja ya juu ya Mkonge na kupungua kwa madaraja ya chini kama ilivyoelezwa katika taarifa za uzalishaji hapo juu.

- Kuhakikisha mitambo ya usindikaji inakuwa katika uimara wa utendaji kwa nyakati zote na pale inapotokea hitilafu kushughulikiwa kwa haraka. Hii inajidhihirisha katika taarifa ya ukarabati wa mitambo iliyoambatishwa na taarifa hii na ufanisi uliopelekea madaraja ya juu kuzalishwa kwa wingi na kupunguza madaraja ya chini.

- Kukamilisha upanuzi wa vichanja vya kuanikia singa ilikuongeza ufanisi katika shughuli za uzalishaji katika viwanda vyote.

- Kurejesha ari ya wafanyakazi viwandani kote kufanya kazi kwa moyo kwakuwa maslahi yao yanazingatiwa na kulipwa kama inavyostahili na kwa wakati.

- Kuweza kulipa stahiki zote muhimu kwa Serikali hususani kodi zote zinazohitajika kwa mujibu wa Sheria.

## 4.0. CHANGAMOTO ZA UZALISHAJI

Katika kipindi cha mwezi Januari hadi mwezi Disemba, 2022, kumekuwa na changamoto na mbali mbali ambazo zimepelekea kutofika malengo ya uzalishaji kama ilivyokusidiwa katika malengo ya uzalishaji kwa Kampuni. Changamoto kubwa ambazo zilijitokea katika kipindi kilichotajwa ni kama ifuatavyo:

- **Changamoto ya Umeme;**

  Kukatika kwa umeme mara kwa mara au umeme mdogo kwa baadhi ya Viwanda

  Hali ya umeme bado imekuwa ni changamoto kubwa sana katika uzalishaji wa viwanda vyetu vyote hasa vile vya kusindika mkonge. Hali hii hupelekea kushindwa kufikia malengo .katika kipindi cha mwaka 2021 changamoto ya kukatika kwa umeme mara kwa mara au kukosa kabisa umeme katika viwanda imechukua asilimia 44% ya changamoto zote ukilinganisha kwa mwaka 2022 ikiwa na asilimia 55.

- **Miundombinu mibovu ya barabara na madaraja**,

Hali ya miundombinu ya barabara za mashambani si shwari na kusababisha wakulima kushindwa kufikisha majani ya Mkonge kwa wakati katika viwanda kwaajili ya usindikaji. Barabara nyingi ziliharibika katika nyakati za mvua na kupelekea kuwepo kwa mashimo na mifereji na kushindwa kupitika kirahisi.

Pia kwa upande wa kiwanda cha Usambara katika nyakati za mvua nyingi inapelekea kiwanda kushindwa kupata majani ya kusindika kutokana na changamoto ya daraja (eneo la daraja) kushindwa kupitika kirahisi.

- **Matengenezo ya mitambo ya kusindikia majani ya mkonge**,

Ukarabati mkubwa wa mitambo ulipelekea kusimamisha uzalishaji kwa kipindi kisichopungua mwezi mmoja kwa kiwanda husika. Aidha, kutokana na mitambo yote kuwa ni kuu kuu kulikua na hali ya kuharibika kwa mitambo hiyo katika hali zisizotarajiwa kulingana na ratiba na mpango wa matengenezo.

- **Mabadiliko ya hali ya hewa**

katika kipindi cha mwaka 2022 kumekuwa badiliko kubwa la hali ya hewa (kiangazi) kilichoweza kuleta athari katika namna mbili, moja kukauka kwa majani na kupelekea usindikaji kuwa mgumu kutokana na mkonge kuwa mkavu na kusababisha uwepo wa taka nyingi kwenye mifereji ya taka. Hali hii inapelekea kupungua uzalishaji kwa kiasi na ubora hivyo kuathiri mapato ya mkulima lakini pia inaathiri ufanisi wa mitambo na kuongeza gharama ya uchakavu hii inaathiri pato la Kampuni.

Pia ukame mwingi umesababisha kukauka kwa vyanzo vya maji ambavyo hutumika katika kusukuma taka na kuoshea singa, hivyo ikapelekea kampuni kuingia gharama kubwa ya kukabiliana na hali hiyo ili kunusuru uzalishaji pia imeathiri malengo ya uzalishaji. Kwa mfano, Kampuni ililazimika kuchimba kisima katika kiwanda cha Magunga na kusafisha kisima cha

zamani kwenye kiwanda cha Magoma Kulasi na kununua pampu 3 mpya ambavyo vyote hivyo havikuwa katika mipango ya kampuni kwa mwaka 2022.

- **Wafanyakazi wa uzalishaji**,

  Kumekuwa na changamoto ya upatikanaji wa wafanyakazi hasa msimu wa kilimo ukifika au pale inapotokea uzalishaji umesimama kupisha matengenezo ya mitambo wafanyakazi wanapotea na inachukua muda na gharama kuwarejesha. Wafanyakazi wengine wamekuwa wakikimbia kazi wakilalamika kwamba kazi ya Mkonge ni ngumu hasa katika usindikaji.

- **Kuchelewa kuletwa majani kiwandani**.

  Usindikaji unategemea majani ya mkonge yaletwe kiwandani kutoka kwa mkulima kupitia Chama chake cha Ushirika, ila kuna wakati inatokea majani yanachelewa kuletwa kiwandani au hayafiki kabisa au yanafika machache kwa kulinganisha na lengo la siku. Hii inapelekea aidha kuchelewa kuanza kazi au kushindwa kufanya kazi kabisa katika siku husika hivyo kushindwa kutimiza malengo ya Mkulima na Kampuni.

- **Kucheleweshwa kwa malipo ya usindikaji**

Hii ni changamoto inayo kwamisha uendeshaji wa viwanda, ambapo baadhi ya AMCOS kucheleweshwa ulipaji wa malipo ya usindikaji isipokuwa Amcos moja ya Magoma tu ndio imekuwa ikilipa malipo ya usindikaji kwa wakati.


Hali hii hupelekea kuchelewa kwa ununuzi wa mahitaji ya uendeshaji mfano mafuta, vilainishini na spare za mitambo. Hupelekea ucheleweshaji wa malipo ya wafanyakazi katika viwanda na kupelekea migomo isiyo ya lazima. Kwa mfano inafikia wakati AMCOS inadaiwa ziaidi ya hati za madai (invoice) 3 ijapokuwa mzigo uliozalishwa unakua umeshauzwa na mnunuzi ameuchukua.

Malipo ya usindikaji yakifanyika mapema yatasaidia kuongeza ufanisi wa utendaji kazi kwa upande wa Kampuni ambayo hii italeta manufaa kwa wadau wote wa Mkonge hususani Mkulima, Kampuni na Serikali.

Takwimu ya athari ya uzalishaji imeambatanishwa katika jedwali namba 6 lifuatalo hapo chini ambapo inaeleza changamoto tajwa hapo juu na namna zilizvyoathiri uzalishaji katika kipindi cha mwezi Januari hadi mwezi Disemba 2021 na 2022.

**Jedwali namba 6: Changamoto za uzalishaji na athari zake katika uzalishaji.**

| MATOKEO YA CHANGAMOTO KATIKA UZALISHAJI 2021 | | | | |
|---|---|---|---|---|
| S/NO | CHANGAMOTO | MASAA | METAS | TONS |
| 1 | Umeme | 2,419.92 | 30,249.00 | 916.64 |
| 2 | Kuharibika kwa mitambo | 2,337.81 | 29,222.63 | 885.53 |
| 3 | Mabadiliko ya hali ya hewa (mvua) | 294.74 | 3,684.25 | 111.64 |
| 4 | Kuchelewa/kutofika kwa majani kiwandani | 91.50 | 1,143.75 | 34.66 |
| 5 | Matengenezo ya Mitambo (rehabilitation) | 1,921.30 | 24,016.25 | 727.77 |
| JUMLA | | 7,065.27 | 88,315.88 | 2,676.24 |
| MATOKEO YA CHANGAMOTO KATIKA UZALISHAJI 2022 | | | | |
| S/NO | CHANGAMOTO | MASAA | METAS | TONS |
| 1 | Umeme | 3,353.25 | 41,915.58 | 1,270.17 |
| 2 | Kuharibika kwa mitambo | 870.00 | 10,875.00 | 329.55 |
| 3 | Mabadiliko ya hali ya hewa (Kiangazi cha muda mrefu)) | 1,530.00 | 19,125.00 | 579.55 |
| 4 | Kuchelewa/kutofika kwa majani kiwandani | 198.00 | 2,475.00 | 75.00 |
| 5 | Ucheleweshaji wa malipo ya usindikaji | 87.56 | 1,094.50 | 33.17 |
| JUMLA | | 6,038.81 | 75,485.08 | 2,287.43 |




| | UMEME | KUHARIBIKA KWA MITAMBO | MABADILIKO YA HALI YA HEWA | KUCHELEWA/ KUTOFIKA KWA MAJANI | MATENGENEZO YA MITAMBO (REHABILITATION) | UCHELEWESHAJI WA MALIPO YA USINDIKAJI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 2021 | 34% | 33% | 4% | 1% | 27% | 0% |
| 2022 | 55% | 14% | 25% | 3% | 1% | 1% |

## 5.0. MUELEKEO WA KAMPUNI

Kampuni imeshaanza kufanya upembuzi yakinifu ili kupata muelekeo wa uwekezaji katika viwanda vyake vyote. Upembuzi utahusisha tathmini ya teknologia ya usindikaji inayotumika sasa na kushauri muelekeo wake pia kutathimini tija na kushauri maeneo mengine mapya yanayohitaji kupelekewa huduma ya usindikaji. Aidha, katika kipindi cha mwaka 2023 kampuni imedhamiria kuhakikisha malengo inayojipangia katika usindikaji mkonge inayatimiza na ikiwezekana kuyapita.

## 6.0. HITIMISHO

Kwakuzingatia kwamba Kampuni hii inamilikwa na Tasisi ya Serikali yaani Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), hivyo itahakikisha inasimamia vyema uwekezaji uliofanywa kuwa ni wa tija kwa wadau wake wote kwani rasilimali hiyo ni michango ya wanachama wa NSSF.

Mwisho tunapenda kutoa shukrani zetu za dhati kwa wadau wetu hususani wakulima wa mkonge wa Tanga, AMCOS (Magoma, Mwelya, Ngombezi, Magunga na Hale), Chama cha Wadau wa Mkonge Tanzania (SAT), Bodi ya Mkonge Tanzania, Wizara ya Kilimo, Serikali ya Mkoa wa Tanga na Wilaya ya Korogwe bila kusahau wanahisa wetu ambao ni Bodi ya Wadhamini ya NSSF na watendaji wote wa Sisalana katika sehemu zote kwa kushirikiana katika kufanikisha uzalishaji wenye tija na manufaa kwa uchumi wa Kampuni, Wakulima na Taifa kwa ujumla.

**Mkonge kwa maendeleo ya Mkoa Tanga na Taifa kwa ujumla.**



**Afisa Mtendaji Mkuu**